

Jinsi ya Kupanga Ratiba Nzuri ya Burudani na Kazi

Kwa nini ni vizuri zaidi kutimiza kazi yako kabla ya kujiburudisha?
Daftari hili litakusaidia kupata jibu.



BURUDANI



KAZI



**Mchanga unawakilisha burudani
zako. Mawe yanawakilisha kazi
zako—mambo unayopaswa
kutimiza.**



Jambo kuu

Ikiwa utaweka mawe makubwa ndani ya ndoo na kisha utie mchanga kujaza nafasi zilizoachwa wazi, utafanikiwa kuweka vyote viwili. Lakini ikiwa utatia mchanga ndani ya ndoo kwanza, hutaweza kuweka mawe yote.



Unatanguliza shughuli gani kwanza?

Tazama picha, na kisha tia alama sanduku (A au B)
chini ya mfuatano wa shughuli zinazoeleza wewe ni mtu wa aina gani.



A



Mimi “ninatanguliza mchanga.”



B



Mimi “ninatanguliza mawe.”

Sasa fanya hivi:

Orodhesha kazi zako za kila wiki.

Orodhesha aina za burudani unazopenda. Tia ndani michezo unayopenda kucheza au kuangalia.



Sasa andika orodha nyingine yenye mambo kutoka katika orodha hizo mbili za awali, ukiorodhesha kwanza mambo yaliyo muhimu zaidi kwako. Kisha tia alama sanduku mojawapo ikiwa jambo uliloorodhesha ni “mchanga” au “mawe.”



1	_____	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
2	_____	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
3	_____	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
4	_____	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
5	_____	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
6	_____	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
7	_____	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
8	_____	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
9	_____	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
10	_____	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>



Je, mambo yaliyo mwanzoni mwa orodha yako ni kazi, au ni burudani? Ikiwa ulitanguliza burudani badala ya kazi, huenda ukahitaji kufanya marekebisho kadhaa ili uweze kukamilisha mambo yote.

Ukitanguliza kazi, utaweza kukamilisha mambo muhimu na bado uwe na wakati kwa ajili ya burudani.

“Mhakikishe mambo yaliyo ya maana zaidi.”—Wafilipi 1:10.